
# KAMPENI YA MISITU YA HIFADHI KWA KILA KIJIJI



"Kila kijiji chenye msitu wa asili katika ardhi yake kina haki ya kuanzisha, kumiliki na kusimamia Msitu wa Hifadhi wa Kijiji kwa manufaa ya sasa na ya kizazi kijacho"

## YALIYOMO


1. MUHTASARI 1

2. NI ZIPI FAIDA ZA MISITU YA HIFADHI ZA VIJIJI KWA JAMII NA TAIFA? 4

3. CHANGAMOTO ZA USIMAMIZI WA MISITU ILIYO KWENYE ARDHI YA VIJIJI 10


4. MAPENDEKEZO: NINI KIFANYIKE ILI KUNUSURU MISITU ILIYO KATIKA ARDHI YA VIJIJI? 13


Tamko namba 6 la Sera ya Misitu ya mwaka 1998 limeelekeza; - ***"Misitu ya Vijiji itasimamiwa na serikali za vijiji au mamlaka nyingine zitakazowekwa na serikali za vijiji zenyewe. Misitu ya vijiji itasimamiwa kwa ajili ya uhifadhi au matumizi endelevu kwa kuzingatia Mpango ya Usimamizi wa Msitu husika"***

## 1. MUHTASARI


### 1.1 Kuhusu Rasilimali za Misitu Tanzania


Uhifadhi endelevu wa Misitu huchangia katika malengo 10 (ambayo ni lengo namba 1,2,5,6,7,8,11,12,13 na 15) kati ya Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDGs). Misitu inaweza kufyonza takribani asilimia 30 ya hewa ukaa iliyopo angani inayotokana na shughuli za kibinadamu, hivyo kuikinga dunia dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi. Kwa mujibu wa taarifa za Wakala wa Takwimu wa Serikali ya Tanzania (2017) Misitu huchangia zaidi ya 85% ya nishati, na 75% kwenye ujenzi na kuboresha Maisha ya watu wa vijijini na mijini. Kwa Mujibu wa Taarifa za Wizara ya Maliasili na Utalii (2015), takribani 55% (sawa na hekta milioni 48.1) ya eneo lote la ardhi ya Tanzania ni misitu. Inakadiriwa kuwa asilimia 46 ya eneo lote la misitu lipo katika ardhi ya vijiji kama inavyoonekana kwenye chati hapa chini




## 1.2 Kuhusu Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii Tanzania

Tathmini ya Misitu iliyofanywa na Serikali ya Tanzania mwaka 2015 ilionesha takribani hekta milioni 22 za misitu ambazo ni sawa na asilimia 46 ya Misitu ya Tanzania ipo kwenye ardhi ya vijiji. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya vijiji namba 5 ya mwaka 1999, Serikali za Vijiji zimepewa mamlaka ya kusimamia ardhi yote iliyo ndani ya mipaka ya Kijiji. Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii (USMJ), ni utaratibu wa kisheria wa kurasimisha misitu iliyo katika ardhi ya vijiji, kwa kuanzisha Misitu ya Hifadhi za Vijiji, Misitu ya hifadhi ya jamii (vikundi) au misitu ya hifadhi ya watu binafsi. Utaratibu huu umewekwa kupitia Tamko namba 5 na 6 la Sera ya Misitu ya mwaka 1998 pamoja na vifungu namba 32 hadi 41 na 65 (3), 78 (3) na 97 (1) (b), vya Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2002. Mchakato wa USMJ hutanguliwa na kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Kijiji kwa kuzingatia vifungu namba 12, 13, 22,33 na 35 vya Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 2007, ambapo eneo la Msitu wa Kijiji hutengwa. Tangu mwaka 1986, Serikali ya Tanzania imekuwa ikishirikiana na Wadau wa Maendeleo kama vile, Mashirika ya Maendeleo ya Serikali za Norway (NORAD), Sweden (SIDA) na Denmark (DANIDA), Finland (FINNIDA), Uswis (SDC), Ubelgiji (BTC), Marekani (USAID) na Uingereza (DFID) na Benki ya Dunia (WB) kuanzisha misitu ya Hifadhi za Vijiji yenye takribani hekta milioni 1.4 kufikia mwaka 2019.




## 1.3 Kuhusu Kampeni ya Misitu ya Hifadhi kwa kila Kijiji

**Kampeni ya "Misitu ya Hifadhi kwa kila Kijiji"** ni toleo la pili la kampeni ya misitu, linalofuatia toleo la kwanza la mwaka 2015, lililoandaliwa na wanajamii wanaotekeleza Usimamizi Shirikishi wa Misitu Tanzania, kwa lengo la kuhimiza usimamizi endelevu wa misitu nchini. Toleo hili la pili linatoa muhtasari wa uzoefu, changamoto, na mapendekezo yaliyotolewa na wadau wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii (USMJ), ikiwa ni pamoja na Asasi za Kijamii, ambazo ni wanachama wa MJUMITA, zilizoanzishwa na vijiji vinavyotekeleza Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM) Tanzania. Asasi hizi zina wananchama katika vijiji 452, vyenye takribani wakazi 1,029,215 wanaoshiriki kusimamia zaidi ya hekta milioni 1.8 katika kata 143, wilaya 30 na mikoa 13 ya Tanzania Bara.

Kampeni ya **"Misitu ya Hifadhi kwa kila Kijiji",** ni wito kwa Serikali za Vijiji, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali Kuu, Asasi za Kiraia na Wadau wa Maendeleo, kuwezesha serikali za vijiji kunusuru takribani hekta milioni 17.6 za misitu ambazo bado hazijahifadhiwa kisheria, ikiwa ni karibu asilimia 80 ya hekta milioni 22 za misitu iliyo katika ardhi ya vijiji. Hii ni muhimu kwani kila mwaka zaidi ya hekta 460,000 za misitu hasa ambayo bado haijarasimishwa hufyekwa na kuongeza zaidi ya tani milioni 44 za hewa ukaa kwenye angala la dunia, hali inayochangia mabadiliko ya tabia nchi. Vile vile uvunaji haramu na usioendelevu umeshamiri katika Misitu hii, hali inayoongeza uharibifu zaidi wa misitu na kupoteza mapato mengi ya serikali.

Njia pekee ya kunusuru misitu iliyo katika

ardhi ya vijiji, ni kuirasimisha kupitia utaratibu wa kisheria wa USMJ. Uzoefu wa wadau wa USMJ umeonesha kuwa, Misitu ya Vijiji yenye utaratibu wa uvunaji endelevu hutoa motisha kwa serikali za vijiji na jamii kusimamia misitu vizuri zaidi, na wakati huo huo kuchangia maendeleo ya jamii. Hata hivyo, utekelezaji wa USMJ unakosa msukumo wa kutosha kwani umekuwa ukitegemea zaidi fedha kutoka kwa wahisani. Aidha Tangazo la Serikali namba 417 lililochapishwa mwezi Mei 2019, limeonesha mwelekeo wa kurejesha utatatibu wa uvunaji endelevu katika Misitu ya Hifadhi za Vijiji kwenye Serikali Kuu, hali itakayoondoa motisha kwa jamii kuendelea kuanzisha na kusimamia Hifadhi za Misitu ya Vijiji. Kwa hiyo, jamii inayotekeleza mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu inapendekeza;

i) Kila kijiji chenye msitu wa asili ambao haujarasimishwa katika ardhi yake kiutenge kuwa Msitu wa Hifadhi wa Kijiji na kuusimamia kikamilifu

ii) Wizara ya Maliasili na Utalii kuendeleza mazingira wezeshi ya kisera kwa Serikali za Vijiji kuanzisha na kusimamia Misitu ya Hifadhi za Vijiji kiendelevu, ikiwa ni pamoja na kuondoa vikwazo vyote kwa vijiji kufanya biashara endelevu ya mazao ya misitu vilivyowekwa kupitia Tangazo la Serikali namba 417, la mwaka 2019

iii) Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa kushirkiana na Idara ya Misitu na Nyuki kuanzisha na Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii

iv) Wadau wa Maendeleo kupitia Mifuko ya Kimataifa ya kupambana na mabadiliko ya tabia nchi, kuungana na Serikali ya Tanzania kuwezesha urasimishaji wa Misitu iliyo katika ardhi ya vijiji.

## 2. NI ZIPI FAIDA ZA MISITU YA HIFADHI ZA VIJIJI KWA JAMII NA TAIFA?

### 2.1 Misitu ya Hifadhi za Vijiji inasaidia Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za misitu Tanzania.

Kufikia mwaka 2019, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ilikuwa imetekeleza uazishaji wa takribani, misitu 589 ya Hifadhi za Vijiji inayokadiriwa kuwa na ukubwa wa hekta milioni 1.4. Kati ya mwaka 2014 hadi 2019, serikali ilishirikiana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs); kama vile Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), na Shirika la Kuhifadhi Mpingo na Maendeleo (MCDI) kuwezesha vijiji 105 katika Wilaya za Liwale, Nachingwea, Kilwa, Mtama, Rufiji, Tunduru, Mvomero, Morogoro, Namtumbo na Kilosa, kusimamia kikamilifu


Baadhi ya wajumbe wa kamati ya maliasili ya Kijiji wakiwa katika zoezi la upimaji wa miti






zaidi ya hekta 610,000 za misitu. Huu ni wastani wa zaidi ya hekta 5,800 kwa kila Kijiji. Misitu yote hii ingefyekwa na kuvunwa kiholela kama isingehifadhiwa kisheria kwa kutengwa kuwa misitu ya hifadhi za vijiji. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na *Burgess* na wenzake mwaka 2019, pamoja na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO, 2019), Misitu ya Hifadhi za Vijiji, imeonyesha kuwa na kiwango bora cha usimamizi ukilinganisha na misitu mingine, haswa ambayo bado haijatengwa kuwa hifadhi katika ardhi ya vijiji.

### 2.2 Kuongeza mapato ya Serikali.

Kati ya vijiji 105 vilivyohudumiwa na Halmashauri za Wilaya kwa kushirikiana na TFCG, MJUMITA na MCDI kati ya 2014 na 2019, jumla ya vijiji 67 viliandaa mipango ya uvunaji endelevu wa mazao ya misitu ambapo kati ya hivyo, vijiji 45 viliandaa mipango ya kibiashara kwa ajili ya kufanya biashara endelevu ya mazao ya misitu kwenye eneo lenye ukubwa wa zaidi ya hekta 330,000. Jumla ya miti yenye mita za ujazo 18,947 ilivunwa kiuendelevu kwa ajili ya mbao na mkaa katika vijiji 54 na mapato yaliyopatikana kwa Serikali za Vijiji pekee ni takribani Shilingi za Kitanzania bilioni 3.54. Katika wilaya za Kilosa, Mvomero na Morogoro, vijiji 30 vilitenga takribani hekta 18,409 ambayo ni wastani wa asilimia 13 ya jumla ya hekta 141,610 za misitu ya hifadhi ya vijiji hivi. Kati ya 2015 na 2019, zaidi ya meta za ujazo 10,400 za miti zilivunwa kiuendelevu kwa ajili ya mkaa, na kuleta pato la zaidi ya Shilingi za Kitanzania bilioni 1.9 kwa Serikali za vijiji pamoja na watengenezaji wa mkaa.

### 2.3 Misitu ya vijiji huongeza rasilimali kwa ajili ya shughuli za uhifadhi.

Vijiji vinavyomiliki misitu ya hifadhi za vijiji hutumia wastani wa asilimia 40 hadi 50 ya mapato yanayotokana na msitu kwa ajili ya shughuli za uhifadhi. Katika mwaka wa fedha 2018/19, vijiji 20 kutoka wilaya za Rufiji, Kilwa,



*Kikosi cha Doria ya Msitu wa Hifadhi wa Kijiji wilayani Kilosa katika picha ya pamoja*

Tunduru na Namtumbo, vilitumia takribani Shilingi za kitanzania milioni 280.9 kwa ajili ya Shughuli za usimamizi wa Msitu, ambapo zaidi ya doria 400 zilifanyika. Katika vijiji 105 vilivyohudumiwa na Halmashauri za Wilaya kwa kushirikiana na TFCG, MJUMITA na MCDI kuna zaidi wanakamati 1,500, wakiwepo zaidi ya wanawake 500, ambao hufanya doria angalau mara 2 kwa mwezi; hivyo kuongeza raslimali watu katika shughuli za usimamizi wa misitu nchini.

## 2.4 Misitu ya vijiji huchochea Maendeleo ya Jamii.

Serikali za Vijiji 36 katika Wilaya za Kilosa, Morogoro, Movomero, Kilwa, Rufiji na Tunduru vimewekeza Shilingi za kitanzania bilioni 1.67 zilizotokana na uvunaji endelevu wa miti katika misitu ya hifadhi za Vijiji, kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kati ya mwaka 2014 hadi 2019. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa majengo ya ofisi za Serikali za Vijiji zenye masijala ya ardhi, ujenzi wa zahanati, kulipia bima ya afya kwa wananchi na kamati za maliasili za vijiji, uchimbaji na ujenzi wa visima vya maji, ukarabati wa miundombinu ya barabara, manunuzi ya pembejeo za kilimo kama trekta, na ujenzi wa vyoo vya shule na vyumba vya madarasa. Miradi hii imepunguza gharama za kuhudumia vijiji kutoka Serikali Kuu na mamlaka za Wilaya.






*"Tekta hili ni mali ya Serikali ya Kijiji cha Mtanzamsona – wilayani Rufiji, limenunuliwa mwaka 2019 kutokana na mapato ya biashara endelevu ya mazao ya misitu"*



## 2.5 Biashara endelevu ya Misitu katika Hifadhi za vijiji inachochea uchumi wa viwanda vidogo vijijini.

Kwa kipindi cha mwaka 2017 hadi 2019 vijiji 3 (Likawage, Ngea na Liwaiti) vya Wilaya ya Kilwa viliweza kuchakata magogo yenye meta za ujazo 421 kwa kutumia mashine ya kisasa na kuuza mbao zenye ubora zaidi na kufanikiwa kupata jumla ya mapato ya Shilingi 223,442,200/=, Mafanikio haya yanatokana na juhudi za Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kwa kushirkiana na wadau wa maendeleo kama WWF na MCDI kuwezesha vijiji kununua mashine za kisasa za kuchakata na kukausha magogo. Matumizi ya teknolojia ya mashine za kisasa **huongeza Idadi, ubora na thamani ya mbao kwa kila mita moja ya ujazo ya magogo yanayochakatwa ukilinganisha na misumeno ya mkono:**

- Kutokana na ukali wa meno ya mashine ya kisasa sehemu ndogo ya gogo hupotea kama vumbi wakati wa uchakataji, hivyo idadi za mbao zinazopatikana kwenye gogo moja inaongezeka ukilinganisha na unapotumia misumeno ya mkono. **Kwa mfano, mwaka 2019 kijiji cha Likawage** Wilayani Kilwa kilitumia mashine ya kisasa kuchakata mita za ujazo 167 za miti aina 4 tofauti ambapo idadi ya mbao zilizopatikana ilifikia asilimia 60 ya miti mzima ukilinganisha asilimia 30% tu unapotumia msumeno wa mkono kuchakata kiasi hicho hicho cha miti.
- Hivyo matumizi ya mashine za kisasa husaidia kupunguza mahitaji ya miti, na ukataji wa misitu, kwani magogo machache zaidi hutumika kutoa idadi kubwa zaidi ya mbao ukilinganisha na tunapochakata kwa kutumia misumeno ya mkono.



*Mbao zilizovunwa kwa utaratibu endelevu katika msitu wa Hifadhi wa kijiji cha Liwiti wilayani kilwa zikikaushwa katika kifaa maalum*

- Mbao zinazotokana na mashine za kisasa zinakuwa na thamani kubwa zaidi, kwani huzalishwa kuendana na vipimo anavyohitaji mteja, hazina mikwaruzo, zinakuwa nyororo na haihitaji kupeleka kwenye mashine nyingine kusafishwa na kunyooshwa.
- Mfano mwaka 2019, Kijiji cha Likawage kiliweza kuingiza asilimia 60% zaidi ya mapato kwa kila meta moja ya ujazo wa miti, ikilinganishwa na kama wangechakata kwa kutumia msumeno wa mkono. Kwa kutumia mashine ya kisasa, mita moja ya mti iliingiza Shilingi za 416,000/=, wakati kwa kutumia msumeno wa mkono, kijiji kingepata Shilingi 260,000/= tu kwa kila mita moja.




*Shughuli za Uchakataji wa Magogo kwa Kutumia Mtambo wa Kisasa zikiendelea katika kijiji cha Likawage wilayani Kilwa mwaka 2019*

## 2.6 Uanzishwaji wa Misitu ya vijiji huongeza haki kwa wananchi wa vijijini kumiliki rasilimali na kutatua migogoro ya ardhi.

Kupitia michakato ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu, jumla ya vijiji 105 vimeweza kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kati ya 2010 na 2019. Vijiji 54 vimeweza kujenga masijala ya ardhi, kutatua migogoro ya ardhi na kuanza mchakato wa kutoa hati miliki za kimila. Jumla ya hati miliki za kimila zipatazo 1447 katika Wilaya za Morogoro, Mvomero, Kilosa na Tunduru zimetolewa kati ya mwaka 2018 na 2019. Kwa mfano, katika zoezi la kuandaa hati miliki za kimila Kijiji cha Sautimoja Wilayani Tunduru mwaka 2019, jumla ya migogoro 11 ya mipaka miongoni mwa wananchi ilitambuliwa, ambapo 8 ilitatuliwa na 3 ilibaki katika majadiliano kwenye baraza la ardhi. Palikuwa na malalamiko 9 ya baadhi ya watu kuwanyima wenza wao wa ndoa haki ya kumiliki ardhi ya familia, ambapo yote yalitatuliwa kwa njia ya mazungumzo. Aidha kulikuwa na matukio 4 ya watu kuvamia maeneo ya huduma za jamii, ambao pia yalitatuliwa kwa njia ya mazungumzo. Baadhi ya vijiji vimekuwa vikitenga maeneo mahususi ya malisho, ili kupunguza migogoro kati ya shughuli za hifadhi ya misitu, wakulima na wafugaji.






*"Wanajamii wa Kijiji cha Sautimoja Wilayani Tunduru, wakifurahia vyeti vya Hati Miliki za Ardhi, walizopatiwa wakati wa Sherehe za Mbio za Mwenge 2019". Kijiji cha Sautimoja kinahifadhi Msitu wenye ukubwa wa hekta 21,966*

## 2.7 Uanzishwaji wa Misitu ya Hifadhi za Vijiji Umesaidia kuimarisha utawala bora katika serikali za vijiji:

Kupitia shughuli za usimamizi wa misitu ya Vijiji, zaidi ya wajumbe 4,200 (wakiwepo takribani wanawake 1,500) wa Serikali za Vijiji na kamati za maliasili katika Vijiji 105 vimeweza kujengewa uwezo wa kusimamia rasilimali zake kuendana na misingi ya utawala bora kati ya mwaka 2014 hadi 2019. Katika kipindi cha 2017 hadi 2019, vijiji 22 vinavyosimamia misitu yenye ukubwa wa takribani hekta 240,810, vilikaguliwa na wakaguzi wa ndani katika halmashauri za Rufiji, Kilwa, Tunduru na Namtumbo ambapo dosari zenye jumla ya vipengele 3,186 ziliibuliwa na kutatuliwa. Wakaguzi walipima hali ya utawala bora kwa kutumia vigezo 20, ambapo wastani wa alama za utawala bora uliongezeka kutoka asilimia 35.9 mwaka 2017, hadi asilimia 43.38 mwaka 2018 na asilimia 51.02 mwaka 2019. Mwaka 2019, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali (CAG) ilianza kukagua hesabu za fedha katika vijiji vinavyomiliki misitu, ambapo Vijiji vya Tawi na Nyamwage Wilayani Rufiji vilikaguliwa na kupelekea kuibuliwa kwa hoja mbalimbali zinazosaidia kuimarisha utawala bora.



# 3. CHANGAMOTO ZA USIMAMIZI WA MISITU ILIYO KWENYE ARDHI YA VIJIJI

**3.1 Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Vijiji bado haujapata nafasi ya kutosha katika mipango ya Serikali, na hivyo kufanya shughuli za kuanzisha misitu ya hifadhi za Vijiji kutegemea wahisani kwa kiasi kikubwa.** Vile vile shughuli za usimamizi wa misitu ya vijiji hazipati nafasi ya kutosha katika mijadala ya kitaifa, kwa mfano Bungeni, kwenye mabaraza ya madiwani, kwenye vyombo vya habari na kwenye vyombo vya ukaguzi kama CAG na wakaguzi wa ndani katika Serikali za Mitaa, pamoja na kwenye majukwaa ya kisiasa kama vile kampeni za uchaguzi au mikutano ya vyama vya siasa.

**3.2 Zaidi ya hekta milioni 17.6 sawa asilimia 80 ya eneo lote la takribani hekta milion 22 za Misitu iliyo katika ardhi ya vijiji bado haijawekwa katika hifadhi rasmi kisheria kufikia mwaka 2019**

(Takwimu hizi ni kwa mujibwa wa taarifa za Serikali ya Tanzania 2015, 2017, 2019; na FAO, 2019)**.** Vile vile mchakato wa kutangaza misitu ya vijiji kwenye gazeti la Serikali (gazettement) kama ulivyoainishwa katika kifungu namba 35 cha Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2002 haujatekelezwa kwa kiasi kikubwa.

**3.3 Taarifa za Serikali ya Tanzania za mwaka 2017, zinazonesha kuwa kila mwaka zaidi ya hekta 469,000 za misitu hupotea** kutokana na matumizi holela kama vile ufyekaji kwa ajili ya kilimo cha kuhama hama, na uvunaji haramu. Aidha, mara nyingi vijiji vimekuwa vikilaumiwa kutokana na upotevu wa misitu kwenye ardhi ya vijiji, bila kujali kuwa, upotevu huu unatokea kwenye maeneo ambayo serikali za vijiji hazijawezeshwa kuyarasimisha kuwa hifadhi za vijiji, na kwenye maeneo ya vijiji yaliyokwishatengwa kwa ajili ya shughuli nyingine za kiuchumi hasa kilimo au kutwaliwa kwa ajili ya uwekezaji mkubwa.

**3.4 Uvunaji Usioendelevu na tafsiri isiyo sahihi ya Misitu ya Mataji Wazi *(general land)* katika Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2002.**

Tathmini ya Raslimali za Misitu iliyofanywa na serikali ya Tanzania (2015), ilianisha kuwa takribani hekta 21,975,094 za misitu zilizo katika ardhi ya vijiji kuwa zipo chini ya miliki ya Serikali za Vijiji. Matokeo ya utafiti huu yalizingatia matakwa ya Sheria ya Ardhi ya vijiji namba 5 ya mwaka 1999, ambayo imeelekeza kutokuwepo kwa ardhi ya jumla *(general land)* ndani ya mipaka ya vijiji. Hata hivyo Maafisa Misitu wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), hutafsiri misitu yote ambayo haijarasimishwa kama Hifadhi za Vijiji kuwa ni maeneo ya wazi na kuidhinisha utoaji wa leseni za uvunaji usioendelevu kinyume na kifungu **namba 49 (4) (a) cha Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2002,** ambayo imekataza shughuli za uvunaji wa Mazao ya Misitu kufanyika bila kuzingatia Mpango wa Usimamizi wa Msitu husika. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG, 2012) ilibaini asilimia 96 ya misitu yote Tanzania inasimamiwa bila uwepo wa Mipango ya Usimamizi iliyoidhinsihwa, na asilimia 57 ya maafisa misitu waliohojiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU, 2013) walikiri kutoa leseni za uvunaji katika maeneo ambayo hayana Mpango wa Uvunaji.



*Magogo yaliyokamatwa yamevunwa kinyume cha Sheria na kutaifishwa na serikali ya kijiji cha Mtanzamso-na wilayani Rufiji mwaka 2019.*



**3.5 Uvunaji Haramu na Mapungufu katika Utawala wa Sekta ya Misitu.**

Asilimia 82 ya wadau waliohojiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU, 2013) walieleza kuwepo kwa viwango vikubwa vya uvunaji haramu (usiofuata taratibu) wa mazao ya misitu ukihusisha; uvunaji wa mazao ya misitu bila vibali (71.9%), uvunaji katika maeneo yasiyoruhusiwa (70.3%), uvunaji wa miti inayozidi kiasi kilichopangwa kuvunwa (67.2%) na vitendo vya rushwa katika mchakato wa uvunaji (63.4%); usafirishaji wa mazao ya misitu kwa njia zisizoruhusiwa (73.7%), usafirishaji wa mazao ya misitu bila alama ya nyundo (70.1%), usafirishaji wa mazao ya misitu bila Hati ya Kusafirishia (TP) (69.4%), matumizi ya kibali kimoja cha kusafirishia (TP) zaidi ya mara moja (64.4%), usafirishaji wa mazao ya misitu nyakati za usiku (65.6%) na usafirishaji wa kiasi kikubwa zaidi cha mazao ya misitu kuliko kilichoruhusiwa (62.2%). Hali hii inaonesha uwepo wa mapungufu katika utawala wa sekta ya misitu nchini, ambapo kwa vyovyote vile, misitu ambayo haijahifadhiwa katika ardhi ya vijiji ndio inayoathirika zaidi.

**3.6 Migogoro ya Ardhi:**

Vijiji vingi ambavyo havijatekeleza Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii (USMJ) havijaandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi, hivyo rasilimali za ardhi ya Kijiji hazijarasimimishwa. Hii inaweka zaidi ya hekta milioni 17.5 ambazo hazijarasmishwa katika hali ya uharibifu zaidi kutokana na matumizi holela na migogoro. Aidha, Hata Misitu mingi ya Hifadhi za Vijiji nchini inakabiliwa na migogoro na wafugaji wa kuhama hama, ambayo ni kikwazo kwa vijiji kuhifadhi na kunufaika na rasilimali misitu kwa njia endelevu.

**3.7 Ahadi ya Usimimizi Shirikishi wa Misitu katika ardhi ya vijiji inafifia?**

Tangazo la Serikali GN 417 la Mei 2019 limeonesha mwelekeo wa Serikali kutaka kuhamisha majukumu ya kuandaa mipango ya uvunaji endelevu, Kuidhinisha wateja wa mazao

ya misitu, na Kupanga bei za mazao ya misitu ya Hifadhi za Vijiji kutoka kwenye Serikali za Vijiji na kuyapeleka kwa Serikali Kuu hususani chini ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), hali inayoelekea kupunguza motisha kwa vijiji kuanzisha na kusimamia misitu ya hifadhi za vijiji. Hii itapelekea zaidi ya hekta milioni 17.6 za misitu zilizopo katika ardhi ya vijiji kuendelea kukosa usimamizi madhubuti.

**3.8 Serikali kupoteza mapato kutokana na uvunaji usioendelevu kwenye misitu ambayo haijahifadhiwa katika ardhi ya vijiji:**
Kutokana na uvunaji kufanyika katika maeneo haya ambayo hayajafanyiwa tathimini ya kina na kuandaliwa mpango wa usimamizi na uvunaji endelevu, ni vigumu kudhibiti mchakato wa uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu. Hali hii inaashiria uwezekano wa mapato mengi ya Serikali kupotea, kama ilivyobainishwa kupitia utafiti uliofanywa na Milledge na wenzake mwaka 2007 na utafiti uliofanywa na Lukumbuzya kwa kushirikiana na Sianga mwaka 2016 ambao ulionesha uwezekano wa mapato yanayopotea kufikia 96% ya kiasi kinachotakiwa kukusanywa. Kuna uwezekano kuwa, miti midogo ambayo haijafikia ukubwa unaoruhusiwa kuvunwa kisheria inakatwa, hivyo kuchochea zaidi upotevu wa misitu. Kwa vyovyote vile mapato ya Serikali yataendelea kupungua kutokana na takribani hekta 469,000 za misitu hii kupotea kila mwaka.

**3.9 Tatizo la vijiji vilivyokwishakamilisha mipango ya matumizi ya ardhi na kuanzisha misitu ya hifadhi ya vijiji kugawanywa au kupandishwa hadhi kuwa miji midogo.**
Mara nyingi mchakato wa usimamizi shirikishi wa misitu Tanzania umekuwa ukiathiriwa na tatizo la kugawanya vijiji kabla uhakiki wa mipaka ya vijiji vipya haujafanyika, hali inayosababisha migogoro baina ya vijiji vipya. Hii husababisha gharama mpya za kufuatilia mchakato wa kutatua mgogoro, kurudia zoezi la kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na ya misitu ya hifadhi ya vijiji husika.

**3.10 Kukosekana kwa mkakati madhubuti wa kuhakikisha ushirikiano unakuwepo baina ya sekta za Misitu, Kilimo na Nishati ambazo kwa pamoja zinategemea misitu iliyo katika ardhi ya vijiji.**
Utafiti uliofanywa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG, 2019) ulibaini kuwa takribani asilimia 89% ya uharibifu wa misitu husababishwa na kilimo hasa cha kuhamahama ambacho kwa kiasi kikubwa huhusisha misitu iliyo katika ardhi ya vijiji ambavyo bado havijatengwa kuwa misitu ya hifadhi. Taarifa za Wakala wa Takwimu Tanzania (NBS, 2017) zinaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 85 ya nishati inayotumika Tanzania hutokana na miti. Inakadiriwa zaidi ya tani milioni 1.5 za mkaa zinatumika Tanzania kwa mwaka na kuwa kiasi hiki kitaongezeka mara mbili zaidi kufikia mwaka 2030 (BEST, 2014). Hii inaonesha umuhimu wa sekta za kilimo, nishati na misitu, kushirikiana kwa karibu katika kusimamia misitu yote iliyo katika ardhi ya vijiji ili iweze kutumika kiuendelevu. Hata hivyo, isipokuwa kwa vijiji 30 vinavyotekeleza mradi wa mkaa endelevu (kati ya 2013 had 2019), uzalishaji wa mkaa nchini hufanyika katika misitu iliyo katika ardhi ya vijiji ambayo haina mipango ya uvunaji endelevu.



# 4. MAPENDEKEZO: NINI KIFANYIKE ILI KUNUSURU MISITU ILIYO KATIKA ARDHI YA VIJIJI?

**4.1 Kuweka na kuendeleza mazingira rafiki ya kisera na kisheria:**
Serikali iendelelee kuweka mazingira rafiki ya kisera kwa vijiji kumiliki na kusimamia misitu yote iliyo katika ardhi ya vijiji. Matamko ya kisera namba 5 na 6 yaliyopo kwenye Sera ya Taifa mwaka 1998 na vifungu namba 32 hadi 41, 65 (3), 78 (3) na 97 (1) (b), vya Sheria namba 14 ya mwaka 2002, kuhusu haki za vijiji kusimamia misitu iliyo katika ardhi yao yaendelee kuwepo, na vikwazo vilivyowekwa katika tangazo namba 417 la Mei 2019, viondolewe. Mikakati ya kuandaa sera na sheria mpya za misitu iwe shirikishi na izingatie haki na wajibu wa wananchi kusimamia misitu iliyo kwenye ardhi ya vijiji, kama ilivyokwisha ainishwa katika Sera na Sheria zilizopo.

**4.2 Serikali iandae mkakati wa kitaifa kwa ajili ya kuwezesha kila kijiji chenye misitu katika ardhi yake kuanzisha msitu wa hifadhi wa Kijiji.**
Mkakati huu uambatane na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na kuwezesha utoaji wa hati miliki za ardhi kwa wananchi wote. Mkakati huu uingizwe kwenye mipango ya maendeleo ya kitaifa na kutengewa bajeti kwa ajili ya utekelezaji.

**4.3 Mamlaka za serikali za mitaa ziwezeshwe kusaidia Serikali zote za Vijiji zilizopo kwenye maeneo yao kuanzisha misitu ya hifadhi za vijiji.**
Mkakati huu uambatane na kuweka utaratibu wa kila Halmashauri kutenga bajeti kwa ajili ya kuendeleza shughuli za usimamizi wa misitu ya hifadhi za vijiji.

**4.4 Serikali iweke utaratibu mahususi wa kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza usimamizi shirikishi wa misitu.**
Hii ni pamoja na kuendeleza Mfuko wa Taifa wa Misitu (TaFF), kuhimiza vijiji vinavyofanya biashara endelevu ya mazao ya misitu kuwekeza katika kueneza mafanikio yao kwenye vijiji jirani, kuhimiza taasisi za kifedha kuwekeza katika misitu ya vijiji, na kuweka utaratibu mahususi wa kuandaa maandiko ya miradi ya usimamizi wa misitu ya vijiji kwa ajili ya kuomba fedha kutoka kwenye mifuko ya kimataifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

**4.5 Sera za viwanda ziambatane na Serikali kuhimiza matumizi ya teknolojia kwenye mnyororo wa thamani wa biashara ya mazao ya misitu.**

Hii ni pamoja na kuhimiza matumizi ya teknoljia katika uchakataji wa magogo, ili kuongeza idadi ya mbao zinazoweza kupatikana kwa kila gogo linalochakatwa, pamoja na kuongeza ubora wa mbao.

### 4.6 Idara ya Misitu na Nyuki (FBD) kwa kushirikiana na Wakala wa Viwango (TBS) waweke viwango vya ubora wa mazao ya Msitu.

Hii itasaidia kudhibiti utakatishaji wa mazao ya misitu yanayovunwa kinyume cha Sheria katika misitu ambayo bado haijahifadhiwa rasmi katika ardhi ya vijiji. Pia serikali ianzishe mfumo wa kidijitali ulio huru na wa wazi wa kufuatilia biashara ya mazao ya misitu.

### 4.7 Serikali izuie kabisa uvunaji wa mazao ya misitu kwenye maeneo ambayo hayajahifadhiwa.

Badala yake ijikite katika kuwezesha vijiji kuandaa mipango ya usimamizi na uvunaji endelevu kwenye maeneo hayo. Ili kuhamasisha uvunaji endelevu kwenye misitu ya Vijiji, Serikali iweke utaratibu mahususi kuwa, miradi ya umma inayohitaji mazao ya misitu kipaumbele kiwe ni kununua mazao hayo kutoka mwenye misitu inayovunwa kiuendelevu katika ardhi ya vijiji.

**4.8 Vyombo vya uangalizi na usimamizi hasa baraza la madiwani, Bunge, na ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), viongeze mikakati ya kuziwajibisha mamlaka zinazohusika katika usimamizi wa misitu**, ikiwa ni pamoja na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa biashara ya mazao ya misitu kwenye ardhi ya kijiji hasa ile ambayo bado haijahifadhiwa. Aidha ukaguzi wa hesabu za fedha za Serikali za Mitaa uambatane na ukaguzi wa hesabu za fedha katika Serikali za Vijiji vinavyofanya biashara endelevu ya mazao ya misitu ili kuhakikisha kuwa rasilimali za vijiji zinasimamiwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.

### 4.9 Serikali iweke mkakati madhubuti wa kuhakikisha kuwa, sera za kilimo, nishati na maji zinatambua umuhimu wa misitu iliyo katika ardhi ya vijiji, kwa ajili ya ustawi wa sekta hizi.


Utekelezaji wa mikakati ya kuendeleza kilimo, nishati na maji, iuwiane na taratibu za usimamizi enelevu wa rasilimali misitu hasa zilizopo katika ardhi ya vijiji.

### 4.10 Serikali iweke sera ya kudhibiti ugawanyaji wa vijiji, au kubadilisha hadhi ya Kijiji kutoka kwenye Halmashauri za Wilaya kwenda kwenye Mji Mdogo.

Endapo vijiji vinagawanywa au vinaingizwa kwenye Manispaa pawepo na utaratibu madhubuti wa kuhakikisha kuwa mipaka ya vijiji husika inakamilika kwa uwazi kabla mabadiliko hayajafanyika. Aidha utaratibu wa mabadiliko uhakikishe kuwa hakutakuwa na athari katika mipaka ya hifadhi ya misitu ya vijiji iliyokwisha anzishwa, au mgawanyo wa raslimali uliokwishawekwa kupitia mpango wa matumizi ya ardhi na mpango wa usimamizi wa msitu wa Kijiji chochote uliokwisha idhinishwa.

### 4.11 Vyama vya siasa viingize mapendekezo yote 4.1 hadi 4.10 hapo juu kwenye ilani zao za uchaguzi wa mwaka 2020.

Mikutano ya kisiasa iambatane na kuhimiza wananchi na wadau kuhifadhi misitu iliyo kwenye ardhi ya kijiji. Katika kipindi cha 2020 – 2025 chama kitachoingia madarakani kielekeze Mamlaka za Serikali kutekeleza mapendekezo haya kwa kuyaingiza kwenye mipango na mikakati ya maendeleo ya serikali.





Jarida hili limeandliwa na mradi wa Haki katika Misitu ambao unatekelezwa na Shirika la Kuhifadhi Misitu wa Asili Tanznaia (TFCG) kwa kushirkiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA). Mradi unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Uingereza kupitia KPMG – Tanzania. Kwa maelezo zaidi kuhusu mradi wa Haki Katika Misitu tafadhali tembelea http://www.tfcg.org/what-we-do/advocate/forest-justice-in-tanzania/


**Kwa mawasiliano zaidi**

Mkurugenzi Mtandaji, Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), S.L.P 23410 Dar es Salaam, Tanzania; Simu: +255 22 2669007; barua pepe: tfcg@tfcg.or.tz; tovuti: http://www.tfcg.org

Mkurugenzi Mtendaji; Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA); S.L.P 21522 Dar-es-Salaam – Tanzania;
tovuti: www.mjumita.org barua pepe: mjumitaorg@mjumita.org
**na**

Mkurugenzi Mtendaji; Shirika la Kuhifadhi Mpingo na Maendeleo (MCDI); S.L.P 49, Kilwa Masoko - TANZANIA Simu: +255 (0) 23 201 3093 / +255 (0)626 475 818; Barua pepe: enquiries@mpingoconservation.org ;
tovuti: http://www.mpingoconservation.org



**Rejea: Toleo hili linaweza kurejewa kama**

TFCG na MJUMITA, (2020), Kampeni ya Misitu ya Hifadhi kwa Kila Kijiji, Dar es Salaam - Tanzania